



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

E-mail Nam. cs.zanzibar@ikubuzanzibar.go.tz
Simu Nam. 2233675/2231823

S. L. P. 437,
ZANZIBAR - TANZANIA

24 JUNI, 2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi amewateua Viongozi wafuatao:-

1. Mhe. Khamis Ramadhan Abdalla ameteuliwa kuwa **Jaji Mkuu wa Zanzibar**. Kabla ya Uteuzi huo Mhe. Khamis alikuwa Anakaimu Wadhifa wa Jaji Mkuu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Rais pia amewateua wafuatao kuwa **Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar**:-

2. Ndugu Salma Ali Hassan. Kabla ya Uteuzi huo Ndugu Salma alikuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).
3. Ndugu Mohamed Ali Mohamed. Kabla ya Uteuzi huo Ndugu Mohamed alikuwa Mrajis wa Mahakama Kuu ya Zanzibar.
4. Ndugu Said Hassan Said. Ndugu Said alikuwa Mwanasheria Mkuu katika Serikali ya Awamu ya Saba ya SMZ.

Aidha, Mheshimiwa Rais amewateua Watendaji wafuatao:-

5. Ndugu Salum Kassim Ali kuwa **Mtakwimu Mkuu wa Serikali**. Kabla ya Uteuzi huo Ndugu Salum alikuwa Katibu Tawala Mkoa wa Kusini Unguja.

6. Dkt. Ali Salim Ali kuwa **Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya UKIMWI Zanzibar**. Dkt. Ali ni Mshauri wa Masuala ya Ukimwi katika Jumuiya ya ZAPHA+.

Uteuzi huo unaanzia leo tarehe 24 Juni, 2022.



(**Mussa Haji Ali**)
KAIMU KATIBU WA BARAZA LA MAPINDUZI
NA KATIBU MKUU KIONGOZI,
ZANZIBAR.